
Ghorofa ya 4, Upande wa Kulia, Jengo la LAPF, Barabara ya Makole
S. L. B. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005
Barua Pepe: info@ewura.go.tz Wavuti: <http://www.ewura.go.tz>

**KANZIDATA YA WAUZAJI NA WATOA HUDUMA KWA SHUGHULI
MBALIMBALI ZA MAFUTA NA GESI ASILIA KWA MWAKA 2018**

1. Kufuatia Kanuni ya 38(1) ya Kanuni za Petroli (Ushiriki wa Watanzania) mwaka 2017, Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji “ijulikanayo kama Mamlaka” inawatangazia watoa huduma, wagavi, na wauzaji wa mafuta na gesi asilia kuwa kanzidata ya watoa huduma kwa mwaka 2018 “LSSP2018” yenye watoa huduma mia moja na sabini na mbili (172) imepitishwa na Mamlaka. Waliopitishwa kwenye kanzidata wanayo haki ya kushiriki kuuza na kutoa huduma kwenye shughuli za mafuta mkondo wa kati na wa chini Tanzania Bara kwa mwaka 2018. Orodha inapatikana kwenye wovuti wa Mamlaka – www.ewura.go.tz.
2. Kwa kutimiza mahitaji ya Kanuni ya 38(1) ya Kanuni za Petroli (Ushiriki wa Watanzania) mwaka 2017, “zijulikanazo kama Kanuni” Mamlaka imeanzisha utaratibu wa kisajili wauzaji na watoa huduma kwenye shughuli za mafuta na gesi asilia kuanzia tarehe 29 Januari, 2018 hadi 31 Machi, 2018. Katika miezi miwili ya usajili, jumla ya wauzaji na watoa huduma mia moja na themanini na mbili (182) kwenye shughuli za mafuta na gesi asilia waliomba kusajiliwa kwenye LSSP2018. Kati yao, wauzaji na watoa huduma kumi (10) hawakuwasilisha taarifa za kutosha kama zilivyooombwa na Mamlaka ili kusajiliwa.
3. Katika kipindi hicho cha usajili, Mamlaka ilihabarisha kila muauzaji na mtoa huduma aliyeomba kusajiliwa kuhusu ukamilifu wa taarifa na kumbukumbu zailizohitajika kwa usajili. Kwa wale waliowasilisha taarifa zisizokuwa kamilifu walishahuriwa kuzikamilisha ipasavyo ili wasajiliwe. Baadhi yao walirekebisha taarifa zao na tayari wamesajiliwa. Wengine, hadi leo hii bado hawajaboresha taarifa zao.
4. Wauzaji na watoa huduma ambao bado wamekosa sifa za kusajiliwa kwenye kanzidata ya LSSP2018, wanakumbushwa kukamilisha zoezi la kurekebisha taarifa zao na kuziwasilisha kwenye Mamlaka kabla ya tarehe 30 Juni, 2018 ili wasajiliwe kutoa huduma mwaka wa 2018.
5. Kanzidata ya LSSP ni muhimu sana kuwezesha watanzania wenye uwezo na ari kushiriki katika miradi ya kitaifa katika mkondo wa kati na chini wa shughuli mafuta na gesi asilia katika Tanzania Bara. Haitakuwa rahisi kwa yeyote kupata bahati ya kutoa huduma kwenye miradi ya kitaifa endapo jina lako halitakuwa kwenye Kanzidata ya LSSP.
6. Wakati matayarisho ya kanzidata ya LSSP kwa watoa huduma kwenye shughuli za mafuta na gesi asilia ni matakwa ya kisheria, ifahamike wazi kuwa usajili haumpi tenda yeyote aliyesajiliwa. Kwa nia ya kushamirisha ushindani na

kuleta tija, itabidi wale wote waliosajiliwa washindanishwe na waendesha miradi ili kupata mtoa huduma bora kutoka kwenye kanzidata ya LSSP ili apewe tenda.

7. Mamlaka inatambua uwepo wa kanzidata kadhaa kwenye wavuti mbalimbali ambazo zimeunganishwa kwenye kanzidata ya LSSP kama vile- www.uwezes haji.go.tz; www.crb.go.tz; www.erb.go.tz; www. ambapo wote walioorodheshwa kwenye kanzidata hizo wanashauriwa kujisajili kupitia EWURA ili waweze kufanikiwa kuwa kwenye kikundi cha watanzania waliotayari kutoa huduma katika shughuli za miradi ya mafuta na gesi asilia.

8. Aidha, Mamlaka inatoa taarifa kwa umma kuwa usajili kwenye kanzidata ya LSSP2018, Awamu ya II unaendelea kuanzia tarehe 1 Mei 2018. Endapo kutakuwepo maswali usisite kuyaelekeza kwenye anwani hii hapa -

Mkurugenzi Mkuu,

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji,

Ghorofa ya 4, Upande wa Kulia , Jengo la LAPF, Barabara ya Makole,

S. L. B. 2857, Dodoma, Tanzania

Simu: +255-26 2329002-3; Nukushi: +255-26 2329005

Barua Pepe: info@ewura.go.tz Wavuti: <http://www.ewura.go.tz>